TANGAZO LA SERIKALI Na. 308 la tarehe 28/4/2023

SHERIA YA MIPANGOMIJI
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA ENEO LA IDODI YA MWAKA 2023

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kurasimisha Makazi Yasiyopangwa Eneo la Idodi ya mwaka 2023.

Utangazaji wa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji la mpango wa urasimishaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.

Mipangokina ya eneo

3. Mipangokina ya eneo lililoainishwa katika Jedwali inaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la urasimishaji lipo ndani ya mipaka ifuatavyo-

"Mpaka unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P1 yenye majira – nukta 745328MS, 9141203KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini kwa umbali wa kilomita 0.6 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P2 yenye majira nukta 744778MS, 9140859KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi kwa umbali wa kilomita 1.8 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P3 yenye majira - nukta 743307MS, 9139689KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini kwa umbali wa kilomita 1.28 hadi mto Idodi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P4 yenye majira - nukta 742413MS, 9138771KZ; baada ya hapo mpaka unaeleka Kusini kwa umbali wa kilomita 3.2 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P5 yenye majira - nukta 739307, 9137816; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini kwa kufuata korongo la mto hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P6 yenye majira - nukta 738947, 9139109; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini kwa umbali wa kilomita 1.5 kwa kulifuata korongo la mto Idodi hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P7 yenye majira – nukta 740163, 9140035; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazin - Mashariki kwa umbali wa kilomita 1.1 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P8 yenye majira – nukta 741125, 9140621; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini – Mashariki kwa umbali wa kilomita 2.3 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P9 yenye majira - nukta 743334, 914144; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki kwa umbali wa kilomita 1.1 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P10 yenye majira - nukta 744238, 9142186; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki kwa umbali wa kilometa 0.8 hadi barabara ya Iringa - Ruaha National Park kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P11 yenye majira - nukta 744900, 9141689; hadi ulipoanzia"

Dodoma,
17 Machi, 2023

ANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*